



Taarifa Kwa Umma, Alhamisi, 29 July 2010
Acheni matumizi ya lugha chafu: Watumishi na Wafanyakazi wa Afya

Wataalam wa Afya wameonywa kuacha kutumia lugha chafu wanapohudumia wagonjwa kwani kwa kufanya hivyo kunaathiri tabia ya kutafuta matibabu na kuwakatisha tamaa wagonjwa wanaokwenda kupata huduma katika vituo vya huduma za afya vya umma.

Hivi karibuni, Mamlaka ya Mji wa Morogoro ilifanyia kazi malalamiko ya wananchi juu ya watumishi na wafanyakazi wa afya katika vituo mbalimbali vya huduma mkoani humo ambao wamekuwa wakitoa huduma chini ya kiwango na kutoa lugha chafu kwa wagonjwa. Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Mh. Issa Machibya amewaambia wauguzi na waganga katika mkutano kwamba amepokea malalamiko mengi ofisini kwake kuhusu utoaji huduma za afya na unyanyasaji wa wagonjwa.

Lugha chafu kwa wauguzi huthibitisha mmomonyoko wa maadili ya kazi na ukosefu wa wito wa kazi hivyo kushindwa kutekeleza majukumu yao kwa kutoa huduma kwa wagonjwa kwa upendo na unyenyekevu kama ilivyobainishwa katika sera za serikali na Mkataba wa huduma kwa mteja. Sikika inapenda kuwakumbusha watoa huduma hawa kuwa, mawasiliano ni muhimu hasa katika taaluma ya afya kutokana na matokeo yake. Kutokuwepo na mfumo thabiti wa mawasiliano baina ya watoa na watumia huduma kunachangia kwa kiasi kikubwa kupotea kwa muda, kutoelewana, mahusiano mabaya na kukwamisha uboreshaji wa huduma. Katika huduma za afya, mawasiliano ni muhimu zaidi sababu lengo kuu ni kujali wananchi, wagonjwa na afya zao na wala si namba, majengo ama mauzo ya huduma hizo. Hivyo basi, mawasiliano mazuri, duni ama kutokuwepo kabisa mawasiliano kuna athari kubwa kwa watumia huduma.

Sikika inawapongeza wote waliotoa malalamiko yao kwa Mkuu wa Mkoa kwa kuonesha ujasiri na uelewa juu ya wajibu wao katika kutafuta na kutumia huduma za afya, na pia inatoa wito kwa wale ambao hawafahamu kuwa ni haki yao kupata huduma bora za afya kwamba wasiogope kusimama na kutetea haki yao kwani wana mamlaka na sheria inawalinda.

Sikika inasisitiza jamii nzima kutoa malalamiko na matatizo yao kwa mamlaka husika mara tu wanaponyanyaswa ama kusumbuliwa na watoa huduma za afya kupitia masanduku ya maoni, ofisi za malalamiko ama kuripoti kwa uongozi wa vituo vya huduma. Kumbuka kuwa ni haki yako kisheria kusikilizwa.

Sikika inatoa wito kwa watoa huduma za afya kuacha kabisa matumizi ya lugha chafu na inashauri Serikali kuwaadhibu wale wote waliohusika katika kadhia hii ili liwe fundisho kwa wengine.

Mr. Irenei Kiria

Mukurugenzi wa Sikika, P.O.Box 12183 Dar es Salaam,

Simu: +255 222 666355/57, Nukushi: 2668015, Barua pepe: info@sikika.or.tz, Tuvoti: www.sikika.or.tz